

Chura Mpweke



Nakiete Mlaki

Chura Mpweke



Nakiete Mlaki



Toleo la kwanza la kitabu hiki lilichapishwa kwa Kiswahili na Kiingereza na Readership for Learning and Development—**Soma** kwenye mfululizo wake mpya wa Kalamu Ndogo.

Kimeandikwa na Nakiete Mlaki kwenye utafiti na uandishi uliowezeshwa na mradi wa **Soma** wa Watoto na Vitabu uliofadhiliwa na Neil Butcher & Associates

Michoro na usanifu na Marco Tibasima

Kimehaririwa na Demere Kitunga pamoja na Godfrey Mishomari and Latifa Miraji



Hakimiliki ya kitabu hiki inamilikiwa kwa pamoja na wabunifu wake na Kiota cha Simulizi cha Watoto na Vitabu cha **Soma**, ambao wameridhia kuweka baadhi ya haki zao kwenye leseni ya [Creative Commons Attribution 4.0 license](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/). Hii ina maana kwamba, yeyote ana uhuru wa kupakua, kufasiri, kupiga chapa na kusambaza kitabu hiki kwa masharti kwamba anawatambua wenye hakimiliki.

ISBN 978-9976-5637-6-4

Tahariri

Chura Mpweke ni hadithi ya kwanza ya ‘kalamu ndogo’, mfululizo mpya wa **Soma** wa vitabu vya watoto vilizoandikwa na watoto. Vitabu vinne vya kwanza katika mfululizo huu ni zao la mradi wa utafiti na uandishi wa Kiota cha Simulizi cha Watoto na Vitabu, uliofadhiliwa na Neil Butcher & Associates. Kiota hiki ni sehemu ya Mkahawa wa Vitabu wa **Soma**; kinachopokea watoto wa miaka 6 hadi 13.

Mradi huu unachangia juhudi za Shirika la William and Flora Hewlett Foundation za kuimarisha ngazi ya awali ya usomaji; kwa kuwezesha na kuhifadhi taarifa za mafanikio ya miradi ya majaribio na ubunifu katika kuandaa na kusambaza matini bora ya usomaji kwa mfumo wa hakimiliki shirikishi barani Afrika.

Mkahawa wa Vitabu **Soma** ni taswira ya **Soma**. Ni nafasi jumuishi ya usomaji na fasihi kwa burudani, utamaduni na maarifa, iliyoanzishwa mwaka 2008 Jijini Dar es salaam. **Soma** ni shirika lisilo la kiserikali kwa jina rasmi *E&D Readership and Development Agency* hadi mwaka 2019; na baadaye *Readership for Learning and Development*. Dira ya **Soma** ni kuona ‘Vijana na Watoto wa Tanzania kuwa na utamaduni kusomea, kusimuliana hadithi na kujituma’.

Mradi huu ulizingatia uwezo na ubunifu wa watoto. Waliwezesha na waandishi wa vitabu vya watoto, walimu, wahariri, wachoraji na wasanifu, kutafiti, kuandika, kupitia, kuhariri, kudurusu na kupendeleza michoro ya hadithi zao. Hadithi hizi ni za kisasa waizozibua kutoka kwenye ngano za mapokeo, uzoefu wao kama watoto na njozi na matamano yao mbali na muktadha wa sasa. Tunawiwa shukurani za dhati kwa jumuiya hii ya wanafasihi kwa kutufunza. Kwa Lisbeth Levey (Liz) kwa kutuamini. Nel Butcher & Associates kwa kutoa rasilimali za kufanikisha mradi huu na kwa kutuunganisha na Mtandao wa Usomaji wa Awali (Early Literacy Network). Liz, Kirsty von Gogh na Ken Harley kwa kutuhimiza na kututia moyo bila kuchoka.

Tunawashukuru watoto wote walioshiriki, wazazi, walimu na wawezeshaji kutoka Watoto na Vitabu na Vituo vya Uelimishaji vya HK na Sanje kwa kujitoa na uvumilivu wao; wawezeshaji na wataalamu mbalimbali: Godfrey E. Mishomari, mwezeshaji kiongozi wa Utafiti na Uandishi; Gonsalves Mpili, Maria Mrindoko, Latifa Miraji, (wawezeshaji wenza); Patrick Gongwe na Alphonse Mapunda (Wakuu wa Vituo); Nadir Tharani (mwandishi, mchoraji na msanifu wa vitabu vya watoto) aliyeshirikiana nasi katika hatua ya uhariri; na Mohamed Ismail, picha za mnato na video; Paulina George na Inviolata Mwakiwone kwa mchango wao wa mawazo, uendeshaji, kuchukua picha za matukio na kuzisambaza; Mugisha Bassasingohe kwa msaada wa TEHAMA; na Ubongo Kids kwa kutupa uzoefu wao. Hatimaye, vionjo vya mradi huu vinapatikana kwenye tovuti yetu www.somabookcafe.com.

Chura Mpweke imeshika nafasi ya kwanza kati ya hadithi 40 zilizoandikwa na watoto. Michoro ya Marco Tibasima imezingatia maelekezo ya mwandishi, na uhariri ulikuwa kidogo na shirikishi ili kuhuisha sauti mtoto. Idhini ya mzazi na ridhaa ya mtoto vilizingatiwa.

Mapato kutokana na kitabu hiki kama yatakuwepo yatachangia kuendeleza mradi huu. Tuliifanya kazi hii kwa mapenzi. Tunaamini itapendwa pia na wasomaji na waelimishaji; vinginevyo itabakia kuwa hekaya nzuri ya ndotoni.

Demere Kitunga,

Februari 2020, Dar es Salaam.

Kulikuwepo na bwawa lenye kingo zilizopakana na mawanda ya nyasi nyororo. Halikuwa bwawa la kawaida, lilikuwa la kipekee. Upekee gani utajiuliza. Lilikuwa na maua ya kila aina, yenye rangi nyingi kuliko unavyoweza kufikiri. Bwawa lenyewe lilikuwa na maji ya zambarau. Watu wote walikuwa wakikanya, “Yeyote atakayeyagusa au kunywa maji ya bwawa hili, atageuka kuwa chura.”









Na wala si chura wa kawaida, bali chura mwenye uwezo wa ajabu. Kama vile uwezo wa kutoa hewa ya moto wanapopumua, nguvu za kuinua vitu vizito kupindukia, kuruka juu umbali mrefu mara kumi zaidi ya binadamu wa kawaida, uwezo wa kutoa ulimi nje kwa umbali wa zaidi ya meta moja na masaibu mengine mengi.

Vyura wadogo walikuwa na uwezo wa kipekee pia. Uwezo ule ule ambao wanalikuwa nao binadamu kama wangegeuka kuwa vyura. Lakini alikuwepo chura mmoja ambaye daima alijitenga na wenzake. Jina lake ni Zakia. Alijitenga kwa sababu ya uwezo wake wa kuishi nchi kavu na majini. Alionewa na wenzake kwa sababu hiyo. Walimwona kuwa ni legelege, asiye na msisimko.

“Toka hapa, sisi tunacheza na watoto poa tu, sio watu kama wewe,” walisema.

Walikuwa wanamsukuma na kumwita ‘pumbavu’ na ‘taahira’. Zakia alikuwa na huzuni siku zote. Alikuwa anajifungia chumbani kwake na kujilaza kitandani akiwa analia huku ameufunika uso wake kwa viganja vyake.

Zakia hakuwa na kaka wala dada. Kwa hiyo aliwaambia wazazi wake kila kitu kilichomsumbua. Mama yake hakuchoka kumwambia, “Usihuzunike Zakia, wao ndio wanajinyima faida ya kuwa na rafiki mzuri kama wewe.”

“Hivi mimi nina kasoro gani? Kwa nini wananifanyia hivi lakini?” Zakia alijiuliza mara kwa mara.



Bwawa liliendelea kuwa zuri na la kumpendeza. Binadamu nao waliamini kuwa bwawa lile na viumbe waliomo ni hatari kwao. Sio tu kwa sababu maji yake yangewageuza kuwa vyura lakini pia kwa sababu ya uwezo waliokuwa nao vyura wale. Kwa muda mrefu binadamu walijaribu kuliharibu bwawa lile. Lakini hawakufanikiwa. Vyura walijibu mapigo.





Lakini kuna kitu kingeweza kuharibu maajabu ya bwawa hilo. Mchanga wa baharini. Kama binadamu wanaligundua siri hii, viumbe wa bwawani wangeangamia. Sababu ni kuwa, kama mchanga wa bahari ungetawanywa kulizunguka bwawa, vyura wangegeuka kuwa sanamu, maua yangekufa, na maji yangegeuka kuwa ya kijivu.




Siku moja asubuhi, Zakia aliamshwa na sauti kubwa za vyura wenzake waliokuwa wakilia.

“Kumetokea nini?” Zakia alijiuliza kwa hofu. Haraka alikimbia nje kuangalia kuna nini. Ndipo alipojikuta akishuhudia tukio la kuogofya kupita ufahamu.

“Oh! Mungu wangu! Hapana.” alipiga yowe.

Zakia hakuamini macho yake. Maji ya bwawa yalikuwa yamebadilika kuwa ya kijivu. Vyura walikuwa wameganda kama sanamu; na maua yalikuwa yamekufa.



“Hii inatokana na jambo moja tu. Binadamu watakuwa wamegundua jinsi ya kuliangamiza bwawa. Sasa mimi ndiye chura pekee aliyebakia.” alijiambia akiwa nje ya nyumba yao, akilikodolea macho bwawa.

Alianza kulia. Machozi yalitiririka kwenye mashavu yake kama maporomoko ya maji.

“Kwa nini mimi? Kwa nini nimebaki mimi tu peke yangu. Kwa nini sijawa sanamu kama wenzangu?” alijiuliza.

Kadri aliyozidi kujiuliza maswali yale, ndivyo alivyozidi kuwa na hasira. Alianza kuyapiga ngumi yale maji akiwa anawaza jinsi yalivyokuwa na rangi nzuri.






Halafu, yale maji yalibadilika ghafla yakawa ya zambarau tena. Unaweza kubashiri ni kwa jinsi gani Zakia alifurahi na kushituka. “Ndio, ndio, ndio, oh, Mungu wangu!” alipiga kelele na kurukaruka kwa furaha.

“Imekuwaje jambo hili kutokea?” alijiuliza.

“Nitakuwa nimefanya nini hadi maji yakageuka kuwa ya zambarau tena?”



Alivyokuwa anajiuliza maswali, alishika maua yaliyokuwa karibu na bwawa.


“Nakumbuka jinsi maua haya yalivyokuwa mazuri.”

Ndipo maua yale aliyokuwa anayashika yalipozinduka ghafla na kunawiri. Zakia alipata mshituko mkubwa kuliko ule wa kwanza. Aliota matende.

Aligundua kuwa anao uwezo wa kurudisha vitu vilivyoharibika kwenye ubora wake wa awali kwa kuvigusa tu na kufikiria jinsi vilivyokuwa kabla ya kuharibika. Alifurahi sana.

Ndipo alipoanza kuyafufua maua yote yaliyokuwa yamekufa.

Kisha alikaa ukingoni mwa bwawa akiwaza, “Kama ninaweza kuyafufua maua, je nitaweza kuwarudisha vyura wezangu? Kuna njia moja tu ya kupata uhakika. Lazima nijaribu.”





Mara baada ya kufikiria hivyo alimkimbilia mama yake. Kabla hajamfufua alimkodolea macho kwa huzuni, machozi yakimlengalega. Kisha alijaribu kumfufua mama yake.

“Nakumbuka jinsi mama yangu alivyokuwa. Alikuwa anapumua, yuko hai. Halafu mama yake akafumbua macho.

“Mama! Mama! Unanisikia?” Zakia aliuliza.

Mama Zakia aliuliza, “Kwani kumetokea nini?”



Zakia alimsimulia mama yake kila kitu kilichotokea pamoja na uwezo wake mpya aliougundua.

Halafu aliendelea kuwafufua vyura wenzake waliosalia.







Hatimaye, Zakia akiwa na umri wa miaka 15 alichaguliwa kuwa kiongozi wa jumuiya yao ya vyura. Si kwa sababu tu ya uwezo wake bali ni kwa sababu ya ujasiri wake na uwezo wa kufikiri kwa haraka. Basi aliendelea kuiongoza jumuiya yake na bwawa limekuwa hai milele.



Chura Mpweke

Zakia anaishi ndani ya bwawa la ajabu, pamoja na jamii yake ya vyura wa ajabu. Anaamini kuwa kila chura ana karama ya kipekee isipokuwa yeye. Wenziwe wanamsimanga na kumuonea. Anakosa furaha na anajitenga nao. Lakini anaifahamu siri ambayo binadamu wanaweza wakaitumia kuliangamiza bwawa na viumbe waliomo. Je, atafanya nini? Je, atakigundua kipaji chake?

Chura Mpweke (tafsiri ya *The Lonely Frog*) ni kitabu cha kwanza katika “Kalamu Ndogo”, mfululizo wa vitabu vya watoto vinavyochapishwa na **Soma**. Vitabu vinne vya kwanza katika mfululizo huu vinatokana na mchakato wa majaribio ya utafiti na uandishi na watoto uliofanywa na **Soma** mwaka 2019 kwa udhamini wa Neil Butcher & Associates.

Nakiete Mlaki, mwandishi wa *Chura Mpweke* ni msichana wa miaka 13 anayesoma darasa la sita. Nakiete anapenda kusoma, kuandika na kusimuliana hadithi. Pia, anapenda kuchora picha na kupaka rangi. Mchoraji amejitahidi kuzingatia michoro aliyochora mwandishi kusawiri wahusika na mandhari kwa jicho lake. *Chura Mpweke* ni kitabu cha kwanza cha Nakiete kuchapishwa.

Vitabu vingine katika Mfululizo wa Kalamu Ndogo ni:

The Lonely Frog

The Poor Lady

Chungu cha Ajabu

Mbuguma na Nasiru



ISBN 978-9976-5637-6-4